

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KARAGWE



### **MKATABA WA KUPANGISHA UKUMBI WA KITUO RAFIKI CHA VIJANA (ANGAZA)**

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe.....Mwezi wa .....Mwaka.....kati ya **Halmashauri ya wilaya Karagwe** (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama Mpangishaji kwa upande mmoja) na ..... (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mpangaji kwa upande wa pili).

Kwa kuwa Halmashauri ndiye mmiliki wa ukumbi huo ulioko eneo la Kayanga na imeihari kumpangisha mtajwa hapo juu kwa masharti ya mkataba huu.

Kwa kuwa mpangishaji ana mamlaka ya kupangisha taasisi au mtu yeyote ukumbi huo ili kujipatia mapato yake.

Na kwa kuwa mpangaji amekubali kwa hiari yake akiwa na akili timamu kupangishwa kama mpangaji,

#### **Hivyo basi mkataba huu unashuhudia mashariti yafuatayo:**

1. Kwamba mpangaji atatakiwa kulipa kiasi cha Tsh 100,000/= (Laki moja elfu tu.) kwa siku yaani ndani ya masaa 24, katika Account Na ..... au taslimu katika Ofisi ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya na kupewa risiti ya kukiri malipo.
2. Kwamba mkataba huu ni wa kipindi cha siku ..... tu) kuanzia tarehe..... hadi tarehe..... Baada ya muda huo kuisha mkataba mwingine waweza kusainiwa kwa makubaliano na maridhiano ya pande zote mbili.
3. Kwamba eneo la kutekeleza mkataba huu ni katika eneo la ndani au mazingira ya nje ya kituo Rafiki cha vijana (Angaza) Kayanga mjini
4. Kwamba mpangaji atawajibika na uharibifu wowote utakaojitokeza katika pango ambao atasababisha yeye mwenyewe kwa uzembe wake.
5. Kwamba pande zote mbili zinakubaliana kwamba haya ndiyo makubaliano yao na yatapaswa kuheshimiwa na pande zote za mkataba.